HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BUKENE,
S.L.P 518,
NZEGA.
11/12/2020

KUMB.NA.BKNSS/J.I/VOL.2/2021/01

JINA LA MWANAFUNZI .....
SHULE YA MSINGI .....

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA BUKENE WILAYA YA NZEGA</u>

kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Mhula wa tarehe 1I.01.2021 . Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 29/01/2021.

MAMBO YA KUZINGATIA

2.1 Sare ya shule ni suruali 2 kwa wavulana na sketi 2 kwa wasichana kitambaa cha bluu bahari kizito. Shati/blauzi nyeupe mikono mifupi, Tai pamoja na sweta la bluu
- Kwa wavulana suruali pana ya marinda inayovaliwa kiunoni.
- Kwa wasichana sketi ya **marinda makubwa ndefu**
- Kwa wanaovaa hijabu ni suruali ya bluu bahari **pana na hijabu rangi nyeupe na blauzi nyeupe ndefu ya mikono mirefu.**
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba kisigino kifupi.

2.2 Sare ya michezo ni bukta rangi ya bluu bahari kwa wavulana na bukta ndefu rangi ya bluu bahari kwa wasichana na tisheti ya rangi ya bluu kwa wote na raba za michezo.

2.3 Daftari counter book 12, kalamu za wino, penseli na mkebe wa hesabu na madaftari ya kawaida makubwa na **faili.**Mzazi unashuriwa mwanao awe na English-Kiswahili Oxford DICTIONARY

2.4 Chakula cha mchana (mahindi, sukari, mboga nk) utaarifiwa baadaye baada ya makubaliano ya wazazi.

2.5 Vifaa vya usafi utatokanavyo nyumbani utakapoagizwa.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, walimu na wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni ni muhimu.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka wakati wote wa masaa ya kuwa shule na siku za shule.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

i.Wizi **ii.**Uasherati **iii.**Ulevi na utumiaji madawa ya kulevya,bangi, n.k **iv.**Ubakaji **v.**Kupigana na kupiga.**vi**.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma **vii.**kudharau bendera ya Taifa .**viii**.Kuoa au kuolewa.**ix.**Kupata mimba au kuharibu mimba **x.**Kutoa mimba **xi.**kukataa adhabu kwa makusudi **xii**.Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

MAKOSA MENGINE NI

a) Kuwa mvivu darasani na nje ya darasa b)Kusema uongo c)Kuwa mtoro au mchelewaji d)kupiga kelele darasani e)kupatikana na makosa ya jinai

Adhabu zifuatazo zaweza kutolewa shuleni

i. Kuchapwa viboko visivyozidi sita kwa wakati mmoja matakoni (wavulana) kwa kulala chini, mikononi wasichana kwa kunyoosha mkono bila kukwepesha kwepesha.
ii. Kufanya kazi ngumu kama kuchimba shimo la takataka, kung'oa visiki nk.
iii. Kupewa onyo la maandishi
iv. Kusimamishwa shule kwa muda
v. Kufidia gharama za uharibifu
vi. Kufukuzwa shule.

MAMBO MENGINE MUHIMU

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii utakabidhi kwa Mkuu wa shule mara baada ya kuripoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA

.....

BUSUMBA ENOCK
MKUU WA SHULE

KIAMBATISHO .A

FOMU YA MZAZI KUKIRI KUTEKELEZA MAAGIZO YOTE

Mimi.....mzazi/mlezi wa mwanafunzi..... ninakubaliana na sheria zote za shule, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule, pia naahidi kushirikiana na shule katika kumsaidia mtoto wangu kitaaluma hasa kuhakikisha anahudhuria shule kila siku.

....

Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe

KIAMBATISHO B

KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ..... mwanafunzi wa shule ya sekondari ..... naapa kwamba nitatii sheria zote za shule kwa muda wote nitakapokuwa nasoma shuleni hapa, pia sitashiriki mgomo wa aina yoyote wala kufanya fujo shuleni wala makosa yoyote ya jinai. Endapo nitakwenda kinyume basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu. Aidha naapa vilevile kwamba nitajibidiisha katika masomo kwa nguvu na uwezo wangu wote, hivyo nitahudhuria vipindi vyote darasani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule. Naahidi vilevile kwamba nitakuwa mstari wa mbele kuyatunza na kuyaboresha mazingira ya shule yangu na kwamba mimi mwenyewe binafsi nitakuwa mtanashati na msafi daima. Kinyume na utaratibu hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu.

....

Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

KIAMBATISHO.C
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FROM THE HEADMASTER,
BUKENE SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 518,
NZEGA.
11/12/2020
0765013138

TO THE MEDICAL OFFICER.....

RE..... **(NAME OF THE STUDENT)**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a fulltime student of this school. The examination should include the following categories.

a) Pregnancy .....
b) Hearing.....
c) eye sight.....
d) limbs.....
e) leprosy.....
f) epilepsy.....
g) tuberculosis
h) other serious diseases.....
i) **PART B: CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and considered that he/she is physically and mentally fit/unfit.
Name ..... Signature ..... Date .....

Official Stamp .....